**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA AFYA**

**FUNGU 52**

# MUHTASARI WA HOTUBA YA WAZIRI WA AFYA MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA (MB), KUHUSU MAKADIRIO YA BAJETI YA WIZARA YA AFYA KWA MWAKA 2026/2027

**MEI, 2026**

## MUHTASARI WA HOTUBA YA WAZIRI WA AFYA MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA (MB), KUHUSU MAKADIRIO YA BAJETI YA WIZARA YA AFYA KWA MWAKA 2026/2027

### A. UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika***, baada ya Bunge lako tukufu kupokea taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI, naomba kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la mwaka 2023, Bunge likubali kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya Wizara ya Afya kwa mwaka 2025/2026, na kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo kwa mwaka 2026/2027. ***Mheshimiwa Spika, pamoja na muhtasari huu, naomba hotuba yangu yote iingie katika kumbukumbu ya Bunge lako tukufu kama ilivyo katika kitabu kilichowasilishwa***.

2. ***Mheshimiwa Spika***, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge hili. Kwa namna ya pekee, namshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Afya. Wizara hii inagusa afya, uhai na ustawi wa kila Mtanzania bila kujali jinsi, umri, dini, kabila au hali ya kiuchumi. Ninatambua dhamana hii kubwa na ninaahidi kuitekeleza kwa uadilifu, uzalendo na weledi.

3. ***Mheshimiwa Spika***, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuimarisha diplomasia ya afya na ushirikiano wa Tanzania na nchi rafiki, mashirika ya kimataifa na wadau wa maendeleo, hasa katika kipindi cha changamoto za ugharamiaji wa huduma za afya kutokana na mabadiliko ya sera za nje. Uongozi wake umehakikisha huduma za afya zinaendelea kutolewa bila kuvuruga misingi ya urafiki, heshima na maslahi ya Taifa. ***Kwa mtazamo wa Mwalimu Nyerere, afya ya wananchi ni msingi wa maendeleo ya watu; na kwa mafunzo ya Nelson Mandela, heshima ya binadamu ni kiini cha taifa huru. Hivyo, huduma ya afya tunayojenga ni huduma ya utu, haki na maendeleo.***

4. ***Mheshimiwa Spika***, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuchaguliwa kwa awamu ya pili katika uchaguzi wa Oktoba 2025. Ushindi huo ni ishara ya imani ya wananchi kwa uongozi wake na Serikali kwa ujumla. Nitaendelea kuibeba agenda yake ya kuimarisha huduma za afya nchini kwa kutambua kuwa Afya ni Mali na Afya ni Mtaji, na kwamba Taifa lenye watu wenye afya ndilo Taifa lenye uwezo wa kuzalisha, kujitegemea na kusonga mbele.

5. ***Mheshimiwa Spika***, napenda kuwapongeza viongozi wakuu wa nchi kwa dhamana walizopewa: Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais; Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuchaguliwa tena kuongoza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar; na Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba (Mb) kwa kuteuliwa

kuwa Waziri Mkuu. Naamini miongozo, maelekezo na busara zao zitaendelea kusaidia utekelezaji bora wa shughuli za Serikali, ikiwemo sekta ya afya.

6. ***Mheshimiwa Spika***, nakupongeza wewe binafsi kwa kuchaguliwa kuliongoza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa umahiri na uongozi thabiti unaozingatia kanuni. Nampongeza pia Naibu Spika, Mheshimiwa Daniel Baran Sillo (Mb), Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge, na Waheshimiwa Wabunge wote kwa dhamana ya kuwakilisha wananchi. Kipekee, nawapongeza Mheshimiwa Dkt. Johannes Lukumay (Mb), Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI, na Mheshimiwa Dkt. Zeyana Abdallah Hamid (Mb), Makamu Mwenyekiti, kwa ushauri wao katika kuboresha utendaji wa Wizara.

7. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara ya Afya itaendelea kupokea na kuzingatia ushauri wa Bunge katika kuboresha huduma za afya nchini. Namshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Baraka Leonard, na watumishi wote wa Bunge kwa ushirikiano wao. Vilevile, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi (Mb) kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Afya, na Ndugu Emmanuel Daud Tayari kwa kuteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia dawa na vifaa tiba. Nawashukuru Dkt. Seif Abdallah Shekalaghe, Katibu Mkuu; Ndugu Ismail Hassan Rumatila, Naibu Katibu Mkuu; Dkt. Grace Elias Magembe, Mganga Mkuu wa Serikali; Menejimenti ya Wizara na watumishi wote wa Sekta ya Afya kwa uzalendo, weledi na kujitoa katika kutekeleza majukumu yao.

8. ***Mheshimiwa Spika***, natoa shukrani kwa Wizara na taasisi za Serikali tunazoshirikiana nazo, ikiwemo Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira; Ofisi ya Waziri Mkuu; Ofisi ya Rais - TAMISEMI; Wizara ya Fedha; Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali; na Wizara ya Maji. Ushirikiano wao umechangia upatikanaji wa rasilimali watu, fedha, uratibu wa sekta mtambuka, usimamizi wa huduma za afya ngazi ya msingi, masuala ya kisheria, afya mazingira na maji safi na salama.

9. ***Mheshimiwa Spika***, nawashukuru Wakurugenzi na Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara, ikiwemo MSD, NHIF, TMDA, NIMR, Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Taasisi ya Chakula na Lishe, hospitali za Taifa, Maalum na Kanda, Waganga Wakuu wa Mikoa na Halmashauri, Waganga Wafawidhi, vyuo vya mafunzo, bodi na mabaraza ya kitaaluma. Nawashukuru pia nchi rafiki, mashirika ya kimataifa, sekta binafsi, mashirika ya dini, asasi za kiraia, vyama vya kitaaluma na vyuo vya elimu kwa mchango wao katika kuimarisha huduma za afya, hususan afya ya msingi, miradi ya maendeleo na afua mbalimbali za afya nchini.

10. ***Mheshimiwa Spika***, kwa unyenyekevu mkubwa nawashukuru wananchi wa Jimbo la Rufiji kwa imani na ushirikiano wanaonipa. Ninawaahidi kuendelea kufanya kazi kwa bidii, uadilifu na uzalendo ili kutekeleza ahadi na vipaumbele tulivyokubaliana kwa maslahi ya Rufiji na Taifa. Naishukuru pia familia yangu kwa upendo, uvumilivu,

ushirikiano, dua na maombi yao wakati ninatekeleza majukumu yangu ya kuwatumikia Watanzania.

11. ***Mheshimiwa Spika***, kwa masikitiko makubwa, nitoe pole kwako binafsi, Bunge lako tukufu, familia, ndugu, jamaa, marafiki na wananchi wote kwa kuondokewa na viongozi na wapendwa wetu, wakiwemo Mheshimiwa Jenista Joachim Mhagama, Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi, Mheshimiwa Halima Idd Nassor, Muadhama Polycarp Kardinali Pengo, Mhashamu Bernadin Francis Mfumbusa na viongozi wengine wa dini na madhehebu mbalimbali. Natoa pia pole kwa watumishi wa Sekta ya Afya waliopoteza wenzao na Watanzania wote waliopoteza ndugu zao kutokana na magonjwa, ajali na majanga.

12. ***Mheshimiwa Spika***, kipekee nitoe pole kwa Mkuu wa Mkoa wa Kigoma na wananchi wote walioguswa na ajali ya boti ya tarehe 13 Machi 2026, iliyosababisha Sekta ya Afya kupoteza watumishi saba wa kada za afya waliokuwa kazini wakitekeleza majukumu yao. Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. Amina.

## B. MWENENDO WA BAJETI NA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA SEKTA YA AFYA, 2021/2022 HADI 2025/2026

13. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imetekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Dira ya Taifa 2050, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa, Sera ya Afya ya mwaka 2007, Ilani ya CCM ya mwaka 2025, HSSP V, Mpango Mkakati wa Muda wa Kati, SDGs 2030 pamoja na makubaliano ya kikanda na

kimataifa yenye lengo la kuimarisha huduma za afya kwa wananchi.

14. ***Mheshimiwa Spika***, kwa mwaka 2025/2026, Wizara na taasisi zake zilikadiria kukusanya Shilingi bilioni 819.98; hadi Machi 2026 zilikusanya Shilingi bilioni 593.85, sawa na asilimia 72.42 ya lengo. Katika mwaka huo, Wizara iliidhinishiwa Shilingi trilioni 1.76 na hadi Machi 2026 imepokea Shilingi trilioni 1.11, sawa na asilimia 63; matumizi ya kawaida yalipokea asilimia 76 na miradi ya maendeleo asilimia 56. Fedha za nje kutoka Global Fund, GAVI, Benki ya Dunia, HBF, UNICEF, UNFPA na wadau wengine ziliendelea kusaidia UKIMWI, TB, malaria, chanjo, lishe, damu salama na afya ya mama na mtoto.

## C. MAFANIKIO YA SEKTA YA AFYA KATIKA AWAMU YA SITA

15. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Awamu ya Sita, upatikanaji wa huduma umeongezeka kwa kasi. Vituo vya kutolea huduma za afya vimeongezeka kutoka 10,153 mwaka 2021/2022 hadi 13,683 Machi 2026, ongezeko la vituo 3,530. Zahanati zimeongezeka kutoka 7,189 hadi 8,706, vituo vya afya 956 hadi 1,359, hospitali 404 hadi 475 na vituo vingine 1,604 hadi 3,143. Majengo mapya yameongezwa Muhimbili, KCMC, Mbeya, Benjamin Mkapa, Bugando, Mirembe, Kibongoto, Mtwara na Chato. Serikali pia imejenga hospitali 10 mpya za rufaa za mikoa, kukarabati hospitali kongwe 50, kukamilisha maboma 980 ya zahanati, kujenga vituo vya afya 390, kuongeza mitambo ya oksijeni kutoka 25 hadi 61 na

kujenga nyumba za watumishi zenye kuhudumia familia 540.

16. ***Mheshimiwa Spika***, huduma za dharura zimeimarishwa kwa kuongeza majengo ya EMD kutoka 7 hadi 125 kufikia Machi 2026 na kuzifikisha kwa mara ya kwanza hadi ngazi ya afya ya msingi, ambako zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania hupata huduma. Vitanda vya wagonjwa vimeongezeka kutoka 86,131 hadi 156,932, sawa na asilimia 82, na vitanda vya ICU katika vituo vya umma kutoka 258 hadi 1,647. Uwekezaji huu una maana ya kupokea wagonjwa kwa wakati, kupunguza msongamano na kuimarisha huduma kwa wagonjwa wanaohitaji uangalizi maalum.

17. ***Mheshimiwa Spika***, afya ya uzazi, mama na mtoto imeimarishwa kwa kuongeza wodi za watoto wachanga kutoka 80 hadi 438, vituo vya upasuaji wa dharura kutoka 445 hadi 630, na vituo vya uchunguzi wa awali wa saratani ya mlango wa kizazi kutoka 732 hadi 1,700. Upatikanaji wa dawa muhimu za afya ya uzazi, mama na mtoto umefikia asilimia 85. Mafanikio haya yamechangia kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi kutoka 556 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2016 hadi 104 mwaka 2022, na kuifanya Tanzania kutambuliwa barani Afrika kupitia uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Serikali imedhamiria kupunguza zaidi vifo hivyo kwa asilimia 50 ifikapo mwaka 2030 na kuvuka lengo la dunia la chini ya vifo 70.

18. ***Mheshimiwa Spika***, katika uchunguzi, matibabu na huduma za ubingwa, Serikali imenunua na kusimika vifaa vyenye thamani ya Shilingi bilioni 241.6; MRI zimeongezeka

kutoka 7 hadi 13, CT Scan 12 hadi 45, Digital X-ray 147 hadi 559, Ultrasound 476 hadi 970, CathLab 1 hadi 4, Mini Angio Suite 5, Fluoroscopy 14 na PET CT Scan 1. Huduma za ubingwa na ubingwa bobezi zimeongezeka, zikiwemo upandikizaji figo 170, uloto 57, vifaa vya usikivu 102, nyonga na magoti 3,037, upasuaji wa mgongo 1,688, upasuaji wa ubongo kwa kufungua kichwa 1,208, kuzibua mishipa ya moyo 2,074, tiba ya mionzi ya ndani 10,056, immunotherapy 4,024 na uchunguzi wa saratani kwa PET-CT kwa wagonjwa 731. Huduma hizi pia zimevutia wagonjwa 26,770 kutoka nchi jirani, hivyo kuimarisha tiba utalii na diplomasia ya afya.

19. ***Mheshimiwa Spika***, chanjo zimeendelea kuwa imara. Watoto waliopata Pentavalent dozi ya tatu wameongezeka kutoka 2,093,412 hadi 3,186,979, sawa na ongezeko la asilimia 52.2, na kiwango cha chanjo kimepanda kutoka asilimia 93 hadi 96, juu ya lengo la kimataifa la asilimia 90. Serikali imeratibu ununuzi wa dozi 161,499,930 za chanjo zenye thamani ya Shilingi bilioni 439.9, na hadi Machi 2026 kulikuwa na dozi 20,268,820 kwenye maghala.

20. ***Mheshimiwa Spika***, upatikanaji wa dawa na bidhaa za afya umeimarika. Serikali imetoa Shilingi trilioni 1.4 kupitia MSD; kati yake Shilingi bilioni 150 zililipia madeni, bilioni 141.9 zilitumika kwa dawa za UKIMWI, malaria na kifua kikuu, na trilioni 1.1 kwa bidhaa za afya za vituo. Viwanda vipya 11 vya dawa na vifaa tiba vimeanzishwa, TPI Arusha kinafufuliwa ili kuzalisha dawa za VVU, na lita milioni 1.45 za viuadudu zenye thamani ya Shilingi bilioni 17.5 zimesambazwa katika halmashauri 184.

Upatikanaji wa bidhaa muhimu 382 umeongezeka kutoka asilimia 58 mwaka 2021/2022 hadi asilimia 88 Machi 2026.

21. ***Mheshimiwa Spika***, rasilimali watu zimeimarishwa kwa kuajiri wataalam 53,633 kuanzia mwaka 2021 hadi Machi 2026, na kufanya watumishi wa afya kufikia 182,430. Watumishi 9,039 wameajiriwa kwa mikataba ya muda mfupi kupitia mapato ya ndani. Kupitia Samia Health Super Specialization Scholarship Program, wataalam 2,982 wamepata mafunzo ya ubingwa na ubingwa bobezi, ikilinganishwa na 961 katika kipindi cha 2016/2017 hadi 2020/2021. Bima ya Afya kwa Wote nayo imeanza baada ya sheria kupitishwa Novemba 2023; hadi Machi 2026, Serikali imetoa Shilingi bilioni 48.8, kaya 172,297 zimefikiwa na wananchi 463,228 wamesajiliwa.

22. ***Mheshimiwa Spika***, mafanikio haya si takwimu tu za majengo, vitanda, vifaa na huduma; ni simulizi ya maisha yaliyookolewa, matumaini yaliyorejeshwa na utu wa Mtanzania uliolindwa. Kama ambavyo Mwalimu Nyerere aliamini kuwa maendeleo ya kweli ni maendeleo ya watu, na kama Nelson Mandela alivyotufundisha kuwa heshima ya binadamu ndiyo msingi wa taifa huru, kila zahanati iliyojengwa, kila hospitali iliyoboreshwa, kila mama aliyepata huduma salama na kila mgonjwa aliyepata huduma karibu na nyumbani ni ushahidi kuwa Tanzania inaendelea kujenga taifa lenye afya, usawa, utu na matumaini.

## D. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA AFYA KWA MWAKA 2025/2026

23. ***Mheshimiwa Spika***, katika udhibiti wa magonjwa yasiyoambukiza, mzigo wa wagonjwa umeongezeka kutoka 6,502,913 mwaka 2024/2025 hadi 6,874,308 Machi 2026, na gharama kutoka Shilingi trilioni 1.3 mwaka 2023 hadi Shilingi trilioni 1.8 mwaka 2024. Wizara imeanzisha kliniki 130 za kisukari na shinikizo la damu, na kufanya jumla kufikia 168; huduma za dialysis zimefikia vituo 74 na kuhudumia wagonjwa 3,342. Huduma za saratani zimepanuliwa kupitia mwongozo wa bodi za saratani, uchunguzi katika hospitali za rufaa za mikoa, huduma Mbeya, KCMC, Bugando na Mtwara, pamoja na uzalishaji wa dawa za uchunguzi na matibabu ya saratani kupitia Cyclotron katika Taasisi ya Saratani Ocean Road.

24. ***Mheshimiwa Spika***, huduma za afya ya akili zimefikia wateja 254,932, vituo 16 vya waraibu vimehudumia wateja 17,807 na upatikanaji wa dawa za afya ya akili umefikia wastani wa asilimia 75. Huduma za sikoseli zimepanuliwa; watoto 17,245 wamepimwa, 369 wamegundulika kuwa na ugonjwa na 2,500 kuwa na vinasaba, wagonjwa 42,564 wamehudumiwa na elimu imewafikia zaidi ya wananchi 29,000. Huduma za kinywa na meno zimeongeza viti 26 kufikia 900 na mashine za mionzi, wakati huduma za macho katika mikoa 15 zimewafikia watu 51,940, wakiwemo 17,697 waliofanyiwa upasuaji, 17,715 waliopata tiba dawa, 10,239 waliopata miwani na 6,289 huduma nyingine.

25. ***Mheshimiwa Spika***, katika magonjwa ya kuambukiza, watu 1,624,907 kati ya takriban 1,700,000 wanaoishi na VVU wanajua hali zao, 1,609,078 wameanza ARV na asilimia 98.1 ya waliopimwa wamefubaza makali ya virusi. Kwa wajawazito, 2,080,819 walipimwa VVU kwa mara ya kwanza na 11,445 walibainika kuwa na maambukizi; watoto 23,023 wenye miezi 18 walipimwa na 1,197 kuthibitika; wajawazito 1,995,822 walipimwa kaswende na 8,598 kati ya 8,684 waliobainika walianzishiwa matibabu. Homa ya ini B, TB na ukoma vinaendelea kudhibitiwa, ambapo watumishi wa afya 13,646 wamekamilisha chanjo ya homa ya ini B, visa 41,473 vya TB vimeibuliwa na visa 755 vya ukoma vimebainika.

26. ***Mheshimiwa Spika***, malaria imedhibitiwa kupitia vyandarua 4,567,179, Shilingi bilioni 5.5 kwa viuadudu na pampu 16,000, pamoja na ununuzi wa ALu, RDTs, Artesunate, SP na primaquine kwa lengo la Zero Malaria 2030. Magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele yanaendelea kushughulikiwa: wananchi 3,331,925 wamepata kingatiba ya usubi, watoto 10,414,632 ya minyoo, watoto 6,176,203 ya kichocho, na wagonjwa 1,775 wa mabusha pamoja na 3,125 wa trakoma wamefanyiwa upasuaji.

27. ***Mheshimiwa Spika***, huduma za kinga zimehusisha Penta-3 kwa watoto 2,361,701, HPV kwa wasichana 866,299, vitamini A kwa watoto 9,115,501, kampeni ya Mtu ni Afya, kaya zenye vyoo bora 9,165,833, wahudumu wa afya ngazi ya jamii 1,832 na kampeni ya Zijue Namba Zako. NIMR imetekeleza miradi 119 kati ya 150, na eIDSR imeimarisha ufuatiliaji wa milipuko;

kipindupindu kimedhibitiwa tangu 25 Februari 2026, na visa 153 vya surua pamoja na 253 vya Mpox viliripotiwa bila vifo.

28. ***Mheshimiwa Spika***, PHEOC imekamilika kuratibu dharura za afya. Wasafiri 10,829,772 wamechunguzwa mipakani, 233 wakipelekwa kwa uchunguzi zaidi, 17,734 wamepata chanjo ya homa ya manjano na ofisi mpya tatu za afya mipakani zimeanzishwa. Kwa huduma za tiba, mwaka 2025/2026 vituo vimeongezeka kutoka 12,846 hadi 13,683, na asilimia 85 ya wananchi wanapata huduma ndani ya kilometa tano. Vitanda vimefika 156,932 na uwiano wa 2.3 kwa watu 1,000.

29. ***Mheshimiwa Spika***, wagonjwa 36,996,862 wamehudumiwa; 35,260,883 wa nje na 1,735,979 wa kulazwa. Magonjwa yaliyoongoza ni mfumo wa hewa, UTI, malaria, kuharisha, ngozi, shinikizo la damu na NCDs nyingine. Tiba asili imeimarishwa; dawa 48 zimesajiliwa, sita zimepelekwa kwenye utafiti wa usalama, mbili za kisukari zinafanyiwa utafiti wa ufanisi, na wagonjwa 648 wamehudumiwa katika hospitali jumuishi.

30. ***Mheshimiwa Spika***, huduma za ubingwa mwaka 2025/2026 zimewafikia wagonjwa 4,202,137; huduma kama IVF, upandikizaji figo, vifaa vya usikivu, puto tumboni, meno, goti au nyonga na uloto zimeokoa takriban Shilingi bilioni 3.67 ambazo zingetumika nje. Madaktari Bingwa wa Dkt. Samia wamehudumia wagonjwa 55,300 katika halmashauri 184 na kujenga uwezo wa wataalam 5,585; huduma mkoba zimefikia wagonjwa 77,118, tiba utalii wagonjwa 3,018 na huduma nje ya nchi wagonjwa 4,363.

31. ***Mheshimiwa Spika***, uuguzi na ukunga, unaotoa takriban asilimia 80 ya huduma, umeimarishwa kupitia mafunzo ya wakunga 1,850; jumla ya waliopatiwa mafunzo ni 9,093, vituo 5,884 vinatumia chati uchungu na huduma ya mama mwambata imefika vituo 1,244. Uhakiki ubora umeimarishwa kupitia maandalizi ya taasisi ya ithibati, maabara zenye ithibati kuongezeka kutoka 90 hadi 102, maabara tano za BSL-3 kujengewa uwezo, na KCRI kutambuliwa na Umoja wa Afrika kwa vimelea hatarishi.

32. ***Mheshimiwa Spika***, damu salama imeimarika kwa chupa 273,105 kukusanywa, sawa na asilimia 82 ya lengo. Kanda sita zina ithibati, Mpango wa Taifa wa Damu Salama umepata ISO 17043 na SANAS, na maabara za Mkemia Mkuu zinaendelea kushikilia ISO 17025:2017. Serikali pia imetoa Shilingi bilioni 242.7 kwa ununuzi wa dawa kupitia MSD, upatikanaji wa bidhaa 382 umefikia asilimia 88.8, na hatua za PIAT, Mloganzila Pharmaceutical and Medical Devices Special Economic Zone, Bio-Equivalent Laboratory na ushirikiano na Sartorius zinaweka msingi wa kujitosheleza kwa bidhaa za afya.

33. ***Mheshimiwa Spika***, huduma za afya ya uzazi, mama, mtoto na vijana mwaka 2025/2026 zimeimarika: wanawake 4,626,300 wamepata huduma za uzazi wa mpango, vituo vya upasuaji wa dharura vimefika 630, wajawazito 2,218,640 walihudhuria kliniki, asilimia 98 walijifungulia vituoni, na mashine tiba joto 392 zimesambazwa. Katika rasilimali watu, Serikali imeajiri watumishi 5,000 na kufikisha jumla ya

watumishi wa sekta ya afya 182,430; wataalam 9,039 wameajiriwa kwa mikataba, na Samia Health Super-Specialization Program imefikisha jumla ya wanaofadhiliwa 1,483.

34. ***Mheshimiwa Spika***, katika TEHAMA, Wizara imetengeneza Health Data Universal API ili mifumo ya afya ibadilishane taarifa na kutoa rufaa kidigitali; eHMS inatumika katika hospitali zote 28 za rufaa za mikoa, GOTHOMIS katika asilimia 96 ya vituo vya ngazi ya msingi, na kompyuta 2,758 zimesambazwa katika mikoa yote 26. Bima ya Afya kwa Wote imeanza kwa kaya zisizo na uwezo, ambapo Serikali imetoa Shilingi bilioni 48.8, kaya 172,297 zimefikiwa na wanufaika 463,228 wameanza kupata huduma. Mabaraza na bodi za kitaaluma yamesajili wataalam 14,310, maduka ya dawa 330, watarajali 3,004, vituo 3,643, kushughulikia mashauri 30, kutoa CPD kwa wataalam 102,066 na kukagua vituo binafsi 654.

35. ***Mheshimiwa Spika***, katika miradi ya maendeleo, Wizara imefuatilia miradi 40 ya ujenzi; miradi 27 ipo katika hospitali za rufaa za mikoa na 13 katika hospitali ya taifa, maalum na kanda. Miradi saba imefikia zaidi ya asilimia 90, miradi nane wastani wa asilimia 70, mradi mmoja asilimia 45, na miradi 24 ipo hatua za awali. Miradi hii inahusisha majengo ya huduma za mionzi, wagonjwa wa nje, damu salama, dharura, ICU, mama na mtoto pamoja na hospitali na huduma nyingine muhimu.

36. Serikali imefanya tathmini ya Hospitali ya Taifa Muhimbili na kubaini changamoto za uchakavu wa miundombinu,

kutawanyika kwa majengo, gharama kubwa za uendeshaji na mazingira yasiyoruhusu maboresho ya huduma za ubobezi na teknolojia ya kisasa. Hivyo, Serikali inapanga kujenga Muhimbili mpya ndani ya miaka mitano kwa gharama ya Shilingi trilioni 1.2, ambapo Shilingi bilioni 908.6 ni mkopo wenye masharti nafuu na Shilingi bilioni 292 ni mchango wa Serikali kupitia maandalizi ya eneo, misamaha ya kodi, ushuru na tozo.

37. Ulinganifu wa gharama na miradi 16 kutoka nchi 15 umeonesha kuwa Muhimbili mpya yenye eneo la mita za mraba 115,000 itagharimu Dola za Marekani 1,819 kwa mita ya mraba, ikilinganishwa na Dola 3,000 hadi 7,000 kwa mita ya mraba katika nchi nyingine. Hivyo, Tanzania itapata hospitali kubwa kwa gharama nafuu, chini kwa wastani wa asilimia 42, na hospitali hiyo itapanda kutoka ngazi ya tatu kwenda ngazi ya nne ya huduma kwa vigezo vya kimataifa.

38. ***Mheshimiwa Spika***, mradi wa Muhimbili mpya si mradi wa afya pekee, bali ni uwekezaji wa kimkakati katika uchumi wa kisasa. Utapunguza rufaa za nje, utaongeza tiba utalii, utavutia wawekezaji, mashirika ya kimataifa na vipaji adimu, na utaifanya Tanzania kuwa kitovu cha huduma za afya, biashara na uwekezaji wa kikanda. Kwa ujumla, utekelezaji huu unaonesha dhamira ya Serikali kujenga mfumo wa afya unaojali kinga, ubora, upatikanaji wa huduma, kujitegemea kwa bidhaa za afya, matumizi ya teknolojia na ustawi wa wananchi.

39. ***Mheshimiwa Spika***, kwa kuhitimisha sehemu hii, mwelekeo wa Sekta ya Afya haujajengwa juu ya takwimu peke

yake, bali juu ya wajibu wa kulinda utu wa mwananchi. Tunapoongeza hospitali, tunasogeza haki; tunapozalisha dawa nchini, tunajenga uhuru wa afya; tunapounganisha mifumo ya TEHAMA, tunaharakisha maamuzi ya kuokoa maisha; na tunaposisitiza ubora, tunathibitisha kuwa kila Mtanzania anastahili kuhudumiwa kwa heshima. Hii ndiyo falsafa ya maendeleo ya watu ambayo Mwalimu Nyerere aliisimamia, na ndiyo roho ya utu ambayo Mandela aliikumbusha dunia.

## MAENEO MAHSUSI YA MSISITIZO

40. ***Mheshimiwa Spika***, kwa kuzingatia maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati wa hotuba yake ya kuzindua Bunge hili, Wizara inaendelea kuboresha utoaji wa huduma za afya nchini kwa kuweka mkazo katika maeneo mahsusi ambayo ni: kuboresha mifumo ya ugharamiaji wa huduma za afya; kuhakikisha upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi; na kuimarisha mifumo ya TEHAMA ili iweze kusomana na kupunguza muda mrefu ambao mteja anatumia kupata huduma.

41. ***Mheshimiwa Spika***, baada ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kusaini Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote na usajili wa wanachama kuanza rasmi Januari 2026, hatua inayoendelea ni maboresho ya mifumo ya utoaji huduma, kuendelea kusajili wananchi wasio na uwezo kupitia kaya na kuendelea kutoa elimu ya Bima ya Afya kwa wananchi ili wawe na uelewa wa dhana ya bima ya afya na kujiunga na mifumo ya Bima ya

Afya iliyopo nchini. Hatua hii ni mageuzi makubwa ya kihistoria yanayoweka bayana ukweli kuwa afya si fadhila, si bahati, si upendeleo, bali ni haki ya msingi ya kila Mtanzania. Napenda kulifahamisha Bunge lako tukufu kuwa Bima ya Afya kwa Wote si mradi wa Wizara pekee bali ni ahadi ya Mheshimiwa Rais kwa Taifa na wananchi wote.

42. ***Mheshimiwa Spika***, kufuatia agizo la Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania la kuimarisha uwezo wa nchi katika kuzalisha bidhaa za afya ili kufikia azma ya kujitosheleza kwa asilimia 80 ifikapo mwaka 2030, Wizara itaendelea kukiwezesha kikosi kazi maalum cha Pharmaceutical Investment Acceleration Taskforce (PIAT) kwa ajili ya kuratibu, kuwezesha na kuharakisha uwekezaji wa viwanda vipya vya bidhaa za afya nchini. Aidha, Wizara itaendelea kuhamasisha wawekezaji wa ndani na nje ya nchi pamoja na kuwawekea mazingira rafiki na wezeshi, ikiwemo upatikanaji wa ardhi na miundombinu muhimu, ili kuwavutia kuwekeza katika ujenzi wa viwanda vya bidhaa za afya na kupunguza utegemezi.

43. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha suala la kuimarisha viwanda vya ndani na uwezeshaji wa wazalishaji wa ndani si maneno tu bali ni dhamira thabiti ya Serikali, Wizara imejipanga kuhakikisha MSD inanunua kwanza dawa zinazozalishwa ndani zilizokidhi vigezo vya TMDA kabla ya kwenda kununua nje ya nchi. Lazima tuchukue hatua za ukweli na uwazi ili kuhamasisha na kulinda uzalishaji wa dawa nchini. Nitumie nafasi hii kuwaalika wawekezaji wote wa ndani

na nje ya nchi kuchangamkia fursa hii ya kuwekeza katika viwanda vya bidhaa za afya ili kuunga mkono juhudi na maono ya Mheshimiwa Rais ya kupunguza utegemezi wa bidhaa za afya kutoka nje ya nchi kwani dawa ni tiba, dawa ni ulinzi na dawa ni usalama kwa wananchi na Taifa kwa ujumla.

44. ***Mheshimiwa Spika***, tunafahamu kuwa mifumo ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za afya ni nyenzo muhimu katika kuhakikisha huduma bora zinatolewa kwa wananchi. Ili kuhakikisha hilo, Wizara itaendelea kuhakikisha mifumo ya kielektroniki iliyopo katika Sekta ya Afya inasomana na kubadilishana taarifa pamoja na kuwezesha kutuma, kupokea na kutunza taarifa za wagonjwa katika hospitali za umma na binafsi, kutoa rufaa kidigitali na kuwezesha upatikanaji wa taarifa kwenye mifumo mingine inayohitaji taarifa mbalimbali. Kusimamia matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika kuleta ufanisi ni kutafsiri kwa vitendo maelekezo ya Mheshimiwa Rais ya kutaka mifumo ya Serikali kuwa michache na yenye kusomana.

45. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara ipo kwenye hatua za awali za uanzishaji wa chombo cha kutoa ithibati ya ubora wa huduma katika vituo vyote vya kutolea huduma vya umma na binafsi. Hatua hii itaimarisha ubora wa huduma za afya nchini kwa kuzingatia uwekezaji uliofanywa na Serikali kwenye vituo na hivyo kuwezesha huduma zinazotolewa katika vituo vyetu kutambulika kikanda na kimataifa. Kupitia chombo hiki, Wizara imedhamiria kutoa huduma bora za afya kwa wananchi, ikiwemo kupunguza muda wa mgonjwa kusubiri huduma na

kuhakikisha matumizi ya lugha zenye staha kwa wagonjwa. Vilevile, ithibati zitakazotolewa katika vituo vya kutolea huduma za afya zitawezesha kuvutia wagonjwa kutoka nje ya nchi na hivyo kuimarisha tiba utalii. Malengo yetu ni kuhakikisha vituo vyote vya kutolea huduma za afya kuanzia ngazi ya rufaa ya Mkoa hadi Taifa vinapata ithibati ya ubora ifikapo 2030.

46. ***Mheshimiwa Spika***, kwa kuhitimisha eneo hili, maeneo mahsusi ya msisitizo yanaonesha wazi kuwa safari ya Sekta ya Afya katika kipindi kijacho haitajengwa tena kwa kuongeza huduma pekee, bali kwa kuhakikisha huduma hizo zinakuwa endelevu, zenye ubora, zinazofikiwa na kila mwananchi na zinazolinda utu wa kila mgonjwa. Bima ya Afya kwa Wote inaleta usawa na inalinda familia dhidi ya umaskini unaotokana na gharama za matibabu; uzalishaji wa dawa na bidhaa za afya nchini unaleta kujitegemea, ajira na usalama wa Taifa; mifumo ya TEHAMA inaleta ufanisi, inapunguza urasimu na inaharakisha maamuzi ya kitabibu; na ithibati ya ubora inaleta heshima, uwajibikaji na ushindani wa huduma zetu kitaifa, kikanda na kimataifa. Falsafa inayotuongoza ni rahisi lakini yenye maana kubwa: afya ya mwananchi si gharama, ni uwekezaji; dawa si bidhaa ya kawaida, ni tiba, ulinzi na usalama; taarifa za mgonjwa si makaratasi, ni maisha yanayohitaji uamuzi wa haraka; na ubora wa huduma si anasa, ni haki ya msingi ya Mtanzania. Haya ndiyo mageuzi tunayoyasimamia: afya iwe haki, dawa zizalishwe nyumbani, huduma ziwe za kidigitali, vituo viwe na ubora unaotambulika,

na kila mgonjwa ahudumiwe kwa heshima. Huu si mpango wa kawaida wa kisekta; ni ahadi ya Taifa kwa watu wake kwamba hakuna Mtanzania atakayeachwa nyuma katika kupata huduma bora za afya, na kwamba Tanzania yenye afya bora ndiyo msingi wa Tanzania yenye uchumi imara, utu, matumaini na maendeleo endelevu.

## 47.VIPAUMBELE VYA MPANGO NA BAJETI, MAPATO NA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO VYA WIZARA YA AFYA, KWA MWAKA 2026/2027.

48. ***Mheshimiwa Spika***, vipaumbele na mpango wa wizara ya afya kwa mwaka 2026/2027 umezingatia mipango ya kitaifa na kisekta ikiwemo, Dira 2050, Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2025-2030, hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kufungua Bunge la 13 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Sera ya Afya na Mpango Mkakati wa Sekta ya Afya.

49. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha malengo hayo yanafikiwa, Wizara kwa mwaka wa fedha 2026/2027 imepanga kutekeleza Vipaumbele 11 vya kimkakati pamoja na afua zake zinazolenga kuleta maboresho makubwa katika Sekta ya Afya kama ifuatavyo: -

i. Kuimarisha ubora wa huduma za afya zinazotolewa ili kukidhi viwango vya kitaifa, kikanda na kimataifa

kwa kutekeleza yafuatayo: -

a. Kuvijengea uwezo vituo vya kutolea huduma za afya wa kufanya tathmini ya ubora wa huduma zinazotolewa kwa lengo la kufikia viwango na kupata ithibati za taasisi za ndani na nje ya nchi.
b. Kuharakisha mchakato wa uanzishwaji wa taasisi ya ndani ya kutoa ithibati ya ubora wa huduma katika vituo vya kutolea huduma za afya.
c. Kuhakikisha huduma bora zenye staha na utu zinatolewa kwa wananchi kwa kuendelea kusimamia maadili, usajili wa wataalam, mashauri ya kinidhamu na kitaaluma, ukaguzi na usimamizi shirikishi wa vyuo na vituo vya kutolea huduma za afya.
d. Kuimarisha huduma kwa mteja ikiwemo kupunguza muda wa kusubiri huduma husika, lugha ya mawasiliano, haki na wajibu wa mteja, mfumo wa kushughulikia malalamiko na kutoa mrejesho pamoja na usalama wa huduma zinazotolewa katika vituo vya kutolea huduma za afya.

ii. Kuimarisha mfumo wa ugharamiaji wa huduma za afya nchini ikiwa ni pamoja na kuendelea na utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote kwa

kutekeleza yafuatayo: -

a. Kuimarisha ugharamiaji wa huduma za afya nchini kwa kutumia vyanzo vya mapato ya ndani.
b. Kuendelea na utekelezaji wa Mpango wa Bima ya Afya kwa Wote kwa kusajili wananchi kutoka kaya zisizo na uwezo na zenye uwezo.
c. Kuendelea kutoa elimu kwa jamii ili wajiunge na bima ya afya.
d. Kuimarisha ushirikiano na Sekta binafsi katika kugharamia huduma za afya nchini.
e. Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Sera, Ilani ya Chama Tawala (CCM mwaka 2025-2030), Mpango Mkakati wa Muda wa Kati, mipango ya mwaka, programu na miradi kwa kuzingatia Mipango wa kitaifa, majukumu ya Wizara ili kuweka mipango ya ugharamiaji wa huduma za afya inayotekelezeka.

iii. Kuwezesha na kuharakisha uwekezaji wa viwanda vya ndani ili kuimarisha uzalishaji na upatikanaji wa bidhaa za afya na kupunguza utegemezi kutoka nje ya nchi kwa kutekeleza afua zifuatazo: -

a. Ujenzi wa maabara ya kisasa ya Utafiti wa

Dawa na ununuzi wa vifaa kwa ajili ya uwekezaji katika viwanda vya dawa nchini.

b. Kuhakikisha upatikanaji wa dawa za kufubaza makali ya virusi vya UKIMWI kwa kuwekeza katika uzalishaji wa dawa katika kiwanda cha TPI pamoja na kuvutia wawekezaji wengine wa viwanda vya dawa.

c. Kuendelea kuimarisha upatikanaji wa bidhaa za afya kwa kuboresha mifumo ya maoteo, ugharamiaji, ununuzi, utunzaji na usambazaji wa dawa na bidhaa nyingine katika ngazi zote za utoaji wa huduma za afya.

d. Wizara kwa kushirikiana na mamlaka nyingine itaendelea kuratibu uwekezaji wa viwanda vya dawa nchini ikiwemo kuandaa majukwaa mbalimbali na wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.

e. Kuimarisha ufuatiliaji, uratibu na udhibiti wa usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa na kusimamia uingizaji wa dawa nchini na matumizi sahihi ya *antibiotics*.

iv. Kuimarisha mifumo na matumizi ya TEHAMA ili kuhakikisha upatikanaji na ubora wa huduma za afya kwa kutekeleza yafuatayo:

a. Kuendelea kuimarisha mifumo katika vituo vya kutolea huduma za afya ili kuweza kusomana na kubadilishana taarifa.
b. Kuimarisha afya mtandao ikiwemo *teleradiology, teleconsultation* na elimu ya afya kwa umma.
c. Kuhakikisha mifumo inayotumika katika Sekta ya Afya inapeleka taarifa kwenye kituo kikuu cha kukusanyia na kuhifadhi taarifa (*central data depository)*.

d. Kuimarisha mifumo ya TEHAMA ili kuondokana na matumizi ya karatasi katika kukusanya, kuchakata, kusambaza na kutumia takwimu ili kuwa na taarifa zenye ubora zitakazosaidia kuweka mipango ya kisera yenye uhalisia.
e. Kuimarisha matumizi ya akili unde katika utoaji wa huduma za afya nchini.

v. Kuimarisha huduma za kinga dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza magonjwa ya kuambukiza, magonjwa ya mlipuko, magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele, pamoja na kuimarisha afua za lishe na usafi wa mazingira kwa kutekeleza afua zifuatazo: -

a. Kuhamasisha jamii kupima na kutambua

mapema hali za afya zao na kuchukua hatua stahiki.

b. Kuimarisha ufuatiliaji na udhibiti wa magonjwa ya mlipuko na utoaji wa taarifa kwa wakati kabla hayajasambaa na kusababisha madhara makubwa.

c. Kukamilisha ujenzi wa kituo cha Umahiri wa Elimu ya afya kwa Umma na kusimika mitambo ya kisasa ya TEHAMA na uchapaji ili kuboresha utoaji wa elimu na hamasa za afya kwa umma.

d. Kuendelea na utekelezaji wa Mpango Jumuishi wa Wahudumu wa afya ngazi ya Jamii ikiwemo kuwajengea uwezo na kutoa nafasi 8,000 za ajira mpya nchini.

e. Kuendelea kuboresha na kuhamasisha utoaji wa huduma za chanjo kwa kuweka mfumo wa kielektroniki katika vituo vya kutolea huduma za afya, ununuzi wa majokofu na ufungaji wa vifaa vya kufuatilia mwenendo wa jotoridi kwenye majokofu ya kuhifadhia chanjo.

f. Kuimarisha huduma za kinga tiba dhidi ya magonjwa yasiyopewa kipaumbele katika Halmashauri 19 kwa ugonjwa wa trakoma,

matende na mabusha pamoja na kutoa huduma za utengamao kwa walioathirika.

g. Kuendelea kutekeleza afua za lishe kwa kuelimisha wananchi kutumia vyakula vilivyoongezwa virutubishi ili kupambana na utapiamlo.
h. Kuimarisha huduma ya udhibiti wa magonjwa mipakani kwa kujenga miundombinu ya kuwatenga wahisiwa wa magonjwa ya kuambukiza na ya mlipuko.

vi. Kuimarisha tafiti na matumizi ya matokeo ya tafiti za afya, ubunifu na teknolojia kwa kutekeleza afua zifuatazo: -

a. Kuratibu tafiti katika vituo vya kutolea huduma za afya, taasisi, pamoja na vyuo kufanya tafiti zinazolenga kutatua changamoto za afya nchini.
b. Kutoa huduma za afya kwa kuzingatia ushahidi wa kisayansi unaotokana na tafiti.
c. Kukamilisha tafiti zinazoendelea na kuanza tafiti mpya katika maeneo ya huduma za kinga, tiba, utengamao, mafunzo, huduma za dawa na mifumo ya afya.

vii. Kuimarisha huduma za ukunga, afya ya uzazi, mama na mtoto ili kupunguza vifo vya watoto wachanga na vitokanavyo na uzazi kwa kutekeleza yafuatayo: -

a. Kuhakikisha upatikanaji wa dawa na bidhaa nyingine za afya ya uzazi, mama na mtoto ili kuchochea juhudi za Serikali za kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi na vifo vya watoto wachanga.
b. Kuimarisha huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto kwa kuongeza idadi ya vituo vinavyotoa huduma za watoto wachanga wagonjwa na waliozaliwa na uzito pungufu, vituo vya huduma za kujifungua na vituo vya huduma rafiki ya afya ya uzazi kwa vijana.
c. Kuendelea kuimarisha huduma za ukunga kwa kusisitiza na kusimamia matumizi ya chati uchungu iliyoboreshwa sambamba na kuboresha vyumba vya kujifungulia ili kuwezesha huduma ya mwambata.

viii. Kuimarisha upatikanaji na uendelezaji wa wataalam katika Sekta ya Afya kwa fani za kati, ubingwa na ubingwa bobezi kwa kutekeleza yafuatayo: -

a. Kuongeza programu za mafunzo ya ubingwa na ubingwa bobezi katika kada mbalimbali za afya kwenye maeneo ya kipaumbele kwa utaratibu wa mafunzo ya muda mrefu na SETI kwa kuzingatia sera za kitaifa za utoaji wa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi.
b. Kusimamia ubora wa mafunzo kwa wanafunzi katika vyuo vya afya vya umma na binafsi pamoja na mafunzo kwa vitendo kwa watarajali.
c. Kuendelea kusimamia utoaji wa mafunzo ya afya ya kada za kati katika vyuo vya afya.
d. Kuendelea kuajiri watumishi wa kada za afya katika Sekta ya Afya kwa ajira ya kudumu na mkataba.
e. Kuendelea na uimarishaji na utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa miundombinu katika vyuo vya afya.

ix. Kuimarisha upatikanaji na uendelezaji wa afua za tiba asili na tiba mbadala kwa kutekeleza afua zifuatazo: -

a. Kuwajengea uwezo wataalam wa kada za

afya ili kuimarisha utoaji wa huduma jumuishi za tiba asili katika vituo vya kutolea huduma za afya.

b. Kuongeza wigo wa huduma za tiba asili ikiwemo kujumuisha dawa na huduma nyingine kwenye mfumo rasmi wa afya.
c. Kuanzisha na kuendeleza mashamba ya miti dawa kwa kila kanda ili kuhamasisha uzalishaji endelevu wa dawa za tiba asili.

d. Kununua eneo la kujenga miundombinu ya kituo cha umahiri wa huduma na mafunzo ya tiba asili mkoani Dodoma.
e. Kuendelea kushirikiana na Mataifa na Taasisi nyingine za kimataifa zilizopiga hatua kwenye matumizi ya teknolojia na tiba asili na mbadala.

x. Kuimarisha upatikanaji wa huduma za tiba dhidi ya magonjwa na kuimarisha huduma za ubingwa na ubingwa bobezi na kuvutia tiba utalii nchini kwa kutekeleza afua zifuatazo: -

a. Kuendelea kutoa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi katika hospitali ngazi ya rufaa ya mkoa, kanda, maalum na taifa.
b. Kuanzisha huduma mpya za kibobezi katika

hospitali za rufaa ngazi ya kanda, maalum na taifa ili kupunguza rufaa za wagonjwa nje ya nchi na kuvutia tiba utalii.

c. Kuendeleza kituo cha umahiri cha Afrika Mashariki cha matibabu ya magonjwa ya moyo na mishipa ya damu, upandikizaji figo, upandikizaji wa uloto na kuanzisha kituo cha umahiri cha matibabu ya magonjwa ya kinywa na meno.
d. Kuongeza idadi ya huduma za ubingwa katika hospitali za rufaa za mikoa kutoka nane (8) hadi 17 na kuanzisha huduma tano (5) za ubingwa kwenye hospitali za Halmashauri.
e. Kuimarisha huduma za uchunguzi kwa kuhakikisha uwepo wa vifaa, vifaa tiba na vitendanishi vya kisasa pamoja na kuwajengea uwezo wataalam wa kada za uchunguzi.
f. Kuimarisha huduma za damu salama ikiwemo ununuzi wa vifaa, vifaa tiba na vitendanishi, kuwajengea uwezo watumishi pamoja na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kuchangia damu ili kuokoa maisha.
g. Kuimarisha huduma za uhandisi na matengenezo ya vifaa tiba kwa

kuwaendeleza na kuwajengea uwezo wataalam wa fani hizo.

h. Kuendelea na uimarishaji wa miundombinu ya utoaji huduma katika hospitali za rufaa za mikoa, hospitali za kanda, hospitali maalum na hospitali ya Taifa.

xi. Kuimarisha huduma za afya ya akili, huduma za utengamao hususan kwa watoto, wazee na watu wenye ulemavu kwa kutekeleza afua zifuatazo: -

a. Kuandaa mpango mkakati wa afya ya akili, msaada wa kisaikolojia na kijamii utakaotoa mwelekeo wa utoaji huduma za afya ya akili katika eneo la kinga, tiba na utengamao.
b. Kuendelea kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi wa Sekta ya Afya ili kukuza usalama wa kazi na ustawi wa kiakili kwa watumishi wa afya.
c. Kuendelea kuimarisha huduma za afya ya akili na huduma za kisaikolojia nchini.
d. Kuimarisha huduma za utengamao na huduma za wazee katika vituo vya kutolea huduma za afya.
e.

## 50. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2026/2027

### Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka 2026/2027

51. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2026/2027 Wizara na hospitali zilizo chini yake inakadiria kukusanya kiasi cha Shilingi bilioni mia saba arobaini na saba, milioni mia mbili, elfu tisini na moja, mia mbili tisini na tisa na senti themanini na moja (747,200,091,299.81). Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni sabini na sita, milioni mia moja tisini na tano, laki nane na elfu hamsini, mia saba thelathini na tano na senti hamsini na tatu (76,195,850,735.53) zinatarajiwa kukusanywa kutoka vyanzo vya ndani vya Makao Makuu ya Wizara, Shilingi bilioni mia moja sitini na tano, milioni mia nane na nne, laki moja arobaini na tisa, mia mbili sitini na nne na senti arobaini na saba (165,804,149,264.47) kutoka Hospitali za Rufaa za Mikoa na kiasi cha Shilingi bilioni mia tano na tano, milioni mia mbili, elfu tisini na moja, mia mbili tisini na tisa na senti themanini na moja (505,200,091,299.81) kutoka Taasisi, Hospitali ya Taifa, Maalum na Kanda.

## Matumizi ya Kawaida

52. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara imepanga kutumia kiasi cha Shilingi bilioni mia sita hamsini na mbili, milioni mia mbili thelathini na sita, laki nane sabini na moja elfu (652,236,871,000.00) kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na asilimia 36 ya bajeti iliyotengwa, ambapo kiasi cha Shilingi bilioni mia tano kumi na sita, milioni mia tatu ishirini na tatu, laki tatu hamsini na sita elfu (516,323,356,000.00) ni mishahara ya watumishi wa Wizara, hospitali na taasisi zilizo chini yake na kiasi cha Shilingi bilioni mia moja thelathini na tano, milioni mia tisa kumi na tatu, laki tano kumi na tano elfu (135,913,515,000.00) ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

## Miradi ya Maendeleo

53. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara imepanga kutumia kiasi cha Shilingi trilioni moja, bilioni mia moja arobaini na nane, milioni ishirini na tano, laki moja themanini na saba elfu (1,148,025,187,000.00) ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo sawa na asilimia 64 ya bajeti iliyotengwa. Kati ya fedha hizo, fedha za ndani ni kiasi cha Shilingi bilioni mia saba themanini na tisa, milioni mia nne hamsini na nane, laki sita na tisa elfu (789,458,609,000.00) na fedha za nje ni kiasi cha Shilingi bilioni mia tatu hamsini na

nane, milioni mia tano sitini na sita, laki tano sabini na nane elfu (358,566,578,000.00) ni fedha za nje.

54. ***Mheshimiwa Spika***, jumla ya fedha zote zinazoombwa na Wizara ni kiasi cha Shilingi trilioni moja, bilioni mia nane, milioni mia mbili sitini na mbili, na hamsini na nane elfu (1,800,262,058,000.00) ili kuweza kutekeleza malengo na vipaumbele iliyojiwekea.

| **Na** | **Fungu** | **Matumizi ya Kawaida** | **Miradi ya Maendeleo** | **Jumla** |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 52 | 652,236,871,000.00 | 1,148,025,187,000.00 | 1,800,262,058,000.00 |

55. ***Mheshimiwa Spika***, Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara ya Afya www.moh.go.tz.

56. ***Mheshimiwa Spika***, naomba kutoa hoja.